



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU

Unapojibu tafadhalli taja:

Namba ya Kotesheni:

LGA/061/2021-22/W/35

MWALIKO WA KOTESHENI

Tarehe 23/03/2022

Kwa: .....

1. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mwaka wa fedha 2021/2022 imetenga kutumia kiasi cha fedha kwa ajili ya **UJENZI WA NYUMBA YA MKURUGENZI**
2. Unakaribishwa kuleta Kotesheni yako ya bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezo kwenye Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi (MMK) kama ilivyofafanuliwa katika sehemu II ya nyaraka hizi.
3. Ada ya Vitabu vya Zabuni (Quotation) ni Tsh. 50,000.00. Fedha ya ada hairudishwi. Vitabu vya Zabuni (Quotation) vinapatikana kwa **OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI, HALMASHAURI YA WILAYA MBULU, S.L.P 74, MBULU**
4. Kotesheni zote katika uhalisia wake (original) pamoja na nakala mbili zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na kuwekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa "Kotesheni Na. LGA/061/2021-22/ W/35. Ni lazima zipelekwe kwa **OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI, HALMASHAURI YA WILAYA MBULU, S.L.P 74, MBULU**
5. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni *tarehe 29/03/2022 kabla au ifikapo saa nne kamilii asubuhi*. Kotesheni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wawakilishi wa wazabuni watakaokuwa wamehuduria katika ufunguzi wa zabuni katika ofisi ya **MKURUGENZI MTENDAJI, HALMASHAURI YA WILAYA MBULU S.L.P 74, MBULU, UKUMBI WA HALMASHAURI**
6. Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, kotesheni za kielektroniki, kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa kotesheni, hazitakubaliwa kwa ajili ya kutathminiwa kwa hali yoyote ile.

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe na uzoefu wa kazi za ujenzi usiopungua miaka miwili (2), aoneshe alishafanya kazi wapi (Ambatanisha nyaraka za uthibitisho).
2. Awe amefanya kazi za ujenzi na taasisi za serikali angalau moja (1) na aambatishe uthibitisho (ambatanisha nakala ya mikataba uliyowahi tekeleza)
3. Awe na Cheti cha ufundi kilichosajiliwa
4. Asiwe na kesi au tuhuma yoyote
5. Awe mwadilifu na mwaminifu
6. Awe tayari kufanya kazi kwa kufuata maelekezo ya mhandisi msimamizi wa ujenzi.
7. Aambatishe barua ya Mtendaji wa Kata kuthibitisha kuwa ni fundi na amefanya kazi na taasisi za serikali.
8. Awe amelipa ada ya ufundi kwa Mkurungenzi Mtendaji



MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA

MBULU  
~~MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA~~  
~~HALMASHAURI YA WILAYA~~  
MBULU